

HOTUBA YA MGENI RASMI MKUU WA MKOA WA MWANZA
MHE: JOHN V.K. MONGELLA KATIKA UZINDUZI WA
MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA NCHINI, KWA MKOA WA
MWANZA TAREHE 29/01/2017

Mheshimiwa Robert Vicent Makaramba, Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu

Kanda ya Mwanza,

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu,

Mhe. CP Clodwig Mtweve, Katibu Tawala Mkoa Mwanza,

Mheshimiwa Dkt. Leonard Masale, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela,

Mheshimiwa Marry Tesha Onesmo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana,

Ndugu. Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,

Waheshimiwa Manaibu Wasajili,

Waheshimiwa Mahakimu Wakazi, Wilaya na Mahakama za Mwanzo,

Waheshimiwa Viongozi mbalimbali wa Serikali,

Waheshimiwa Viongozi wa vyama vya Siasa,

Ndugu Viongozi wa dini mliopo,

Mawakili wa Serikali na kujitegemea,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Wanahabari.

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima, na kuniwezesha kushiriki nanyi katika tukio hili muhimu katika historia ya Nchi yetu, ambayo huja mara moja kila mwaka mpya. Aidha ninapenda kumshukuru Mhe. Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, kwa pamoja na watumishi wote wa mahakama ya Tanzania katika Kanda hii kwa kunipa heshima hii ya kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Maadhimisho haya muhimu ya uzinduzi wa wiki ya sheria kwa Mkoa wa Mwanza.

Ndugu wananchi, Maadhimisho haya ya wiki ya sheria nchini yanaashiria kuanza rasmi kwa shughuli za Ki-mahakama ya Tanzania, kama ilivyoielezwa katika Ibara ya 107 A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mahakama ndiyo mhimili pekee uliopewa Mamlaka ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; katika uzinduzi wa shughuli za Mahakama ya Tanzania, kila mwaka kunakuwa na maudhui au kaulimbiu yake,

na katika maadhimisho ya mwaka huu 2017, Kaulimbiu ya maadhimisho ya wiki ya sheria ni **“UMUHIMU WA UTOAJI HAKI KWA WAKATI KUWEZESHA UKUAJI UCHUMI”**.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya mwaka huu 2017 imekuja wakati muafaka kwani kumekuwa na Maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii katika Mkoa wetu na Nchini kwetu, ambapo maendeleo hayo yanaenda sambamba na mahitaji makubwa ya huduma za haki zinazotakiwa kutolewa kwa wakati na Mahakama ya Tanzania kwa wananchi wa Tanzania .

Ndugu wananchi, Huduma za haki humlenga mwanchi ambaye ndiye Mdau wa kwanza. Hivyo basi, ni mategemeo yangu kuwa kauli mbiu/maudhui haya yakitekelezwa vizuri na mhimili huu wa Mahakama ya Tanzania, itasaidia si tu katika kumaliza mashauri mengi ya Mahakama kwa wakati, bali itadumisha amani na utulivu katika nchi yetu, kwani, bila amani na utulivu hakuna maendeleo yoyote nchini.

Ndugu Wananchi, Nina matumaini kuwa wiki ya sheria itakuwa wa mafanikio siyo tu kwa Mahakama bali kwa wananchi wa Mkoa wa Mwanza na taifa letu kwa ujumla kwani kupitia elimu ya sheria itakayotolewa kwenye mabanda ya wadau wa sheria kuanzia leo tarehe 29 Januari, 2017 hadi tarehe 02 Februari, 2017, itaongezwa uelewa kwa wananchi kuhusu sheria, pia wananchi watapata nafasi ya kutoa maoni yao kwani nimearifiwa kuwa kutakuwa na banda maalum la wananchi kutoa maoni yao, na niwaombe mhakikishe maoni hayo yatakayo tolewa yanafanyiwa kazi, kwani Maoni ya wananchi juu ya haki na vyombo vya Haki yanachangia sana katika kuleta mageuzi kwenye utendaji haki.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi, Nimefurahishwa na uamuzi wenu wa kuwashirikisha katika tukio hili wadau mbali mbali wa Mahakama na sekta ya sheria kwa ujumla ikiwa pamoja na Msajili wa hati Kanda ya ziwa, Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Mwanza, kwani changamoto kubwa sana inayotukabili Mkoa wa Mwanza ni kuhusu Migogoro ya ardhi, mfano kwa mwaka 2016 kipindi cha Januari hadi Desemba kwa Wilaya za Nyamagana na Ilemela jumla ya malalamiko/ migogoro ya ardhi 1,040 ilipokelewa, hii ina maanisha kwa kuwa mwaka mzima una siku 365, kila siku ikiwa pamoja na jumamosi na jumapili kwa wastani migogoro mitatu ya ardhi inatokea .

Nimeamua kutumia takwimu kuonyesha ukubwa wa tatizo la migogoro ya ardhi kwani mhesabati mashuhuri "Andreys Dunkels" alisema haya kuhusu takwimu:

"It is easy to lie with statistics, but it is hard to tell the truth without them"

[Ni rahisi kudanganya kwa takwimu, lakini vile vile ni vigumu kusema ukweli bila takwimu]

Mhe. Jaji Mfawidhi, Mahakama Kuu Mwanza, Wahe. Majaji, manaibu Wasajili, Mahakimu na watumishi wote wa Mahakama ya Tanzania Kanda ya Mwanza, napenda niwakumbushe mfumo bora wa utoaji haki ni ule wenye fursa ya haki na unatenda haki sawa na kwa wakati; kwa gharama nafuu; ulio wazi na **unaoaminika na unaoendeshwa na Mafisa na watendaji waadilifu.**

Mwisho, leo tarehe 29/01/2017, natamka rasmi maadhimisho ya wiki ya sheria nchini kwa Mkoa wa Mwanza yamefunguliwa na naomba niwatakie maadhimisho mema ya wiki ya sheria nchini.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.